



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI**



**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA BODI YA ZABUNI  
TAREHE 16/11/2021**

**A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

- |                           |                      |              |
|---------------------------|----------------------|--------------|
| 1. Bw. Joram A. Noa       | - Afisa Uchaguzi     | - Mwenyekiti |
| 2. Bw. Mawazo Masatu      | - Afisa Manunuzi     | - Katibu     |
| 3. Bw. Daudi O. Mlahagwa  | - Afisa Mazingira    | - Mjumbe     |
| 4. Bw. Aristariki Kimario | - Afisa Mifugo       | - Mjumbe     |
| 5. Bw. Juma Mbwelwa       | - Afisa Elimu Msingi | - Mjumbe     |
| 6. Dkt. Hassan Msafiri    | - Daktari            | - Mwalikwa   |
| 7. Bw. Idd Maeda          | - Mhandisi           | - Mwalikwa   |

**B. MWANDISHI**

1. Bi. Manka Hija

**AGENDA NA. HWP/TB/1/1/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwasalimu wajumbe na kumkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti alifungua kikao Saa 5:04 Asubuhi na kuwajulisha wajumbe kuwa Agenda ni moja (1) ya kupitisha mchakato wa manunuzi ya ujenzi wa jengo la ICU Hospitali ya Wilaya Pangani na ujenzi wa nyumba wa watumishi kituo cha Afya Mkalamo pamoja na madarasa 28 Elimu Msingi na Sekondari

**AGENDA NA. HWP/TB/2/1/2021 – MCHAKATO WA MANUNUZI YA UJENZI WA JENGO LA ICU HOSPITALI YA WILAYA PANGANI NA UJENZI WA NYUMBA WA WATUMISHI KITUO CHA AFYA MKALAMO PAMOJA NA MADARASA 28 ELIMU MSINGI NA SEKONDARI**

Katibu aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe inayohusu mchakato wa manunuzi wa ujenzi wa jengo la ICU Hospitali ya Wilaya ya Pangani, ujenzi wa nyumba ya watumishi (three in one) Kituo cha Afya Mkalamo na ujenzi wa madarasa 28 Elimu Msingi na Sekondari kwa mchanganuo ufuatao:-

.....  
  
KATIBU

TAREHE: 16/11/2021

.....  
  
MWENYEKITI


- ✓ ICU na Nyumba ya Mtumishi Mkalamo (three in one) TSh. 365,725,822.51
- ✓ Ujenzi wa madarasa 28 TSh. 560,000,000.00

Baada ya taarifa hiyo kuwasilisha wajumbe kwa pamoja waliipitisha taarifa hiyo bila hoja.


### AGENDA NA. HWP/TB/3/1/2021 – KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alimshukuru wajumbe na kufunga kikao mnamo Saa 5:20 Asubuhi.

**U M E T H I B I T I S H W A:**



MAWAZO MASATU  
KATIBU



JORAM A. NOA  
MWENYEKITI

TAREHE: 16/11/2021